


SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



Maswali

1. Mbona Hezekia alitaka uzaidizi wa Mungu?
2. Nani aliletea Hezekia ujumbe kutoka kwa Mungu?
3. Mungu alitumia Hezekia ujumbe gani?
4. Hezekia alifanya nini baada ya Isaya kuenda?
5. Illichukua muda gani Mungu kujibu maombi ya Hezekia?
6. Mungu alijibu nini?
7. Mungu aliyea Hezekia ishara gani?
8. Isaya aliambia watumishi wafaye nini ili Hezekia apone?
9. Mungu aliyea Hezekia miaka mingapi ya kuishi?
10. Mungu aliweka ahadi kwa Daudi namna gani?

Majibu

1. Hezekia aliuliza uzaidizi kwa Mungu kwa sababu alikuwa mgonjwa sana.
2. Isaya alileta ujumbe kutoka kwa Mungu.
3. Unaenda kufa. Hautapona.
4. Hezekia alilia na kuomba Mungu amkumbuke na amponye.
5. Mungu alijibu Hezekia papo hapo.
6. "Nitakuponya. Kwa muda wa siku 3 utaenda Hekaluni kuabudu."
7. Kivuli cha jua kilirudi nyuma hatua kumi.
8. Isaya aliambia watumishi waweke bandiko ya tini kwa jipu.
9. Mungu alimpa Hezekia miaka mingine 15 ya kuishi.
10. Kwa huo muda wa miaka mingine, Hezekia alipata mwana wa kuwa mfalme. Mungu alikuwa ameahidi Daudi kwamba mmoja wa uzao wake utaendelea kuwa mfalme.

77 Mungu anaponya Hezekia

Kwa Biblia

2 Wafalme 20:1 – 11

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hujibu maombi yetu. Mungu hutimiza ahadi zake

Somo

Hezekia alikuwa mgonjwa sana. Hezekia alikuwa mgonjwa wakati Waashuru walikuwa wakishambulia nchi ya Yuda. Hezekia alikuwa na shida nyingi pamoja na wasi wasi. Ujumbe ulimkujia. Alisikia habari kwamba Waashuru wanashambulia vijiji nya Yuda. Hezekia alikuwa mgonjwa sana kando na shida zingine za kushulikia.

Hezekia aliendelea kuwa vibaya. Hezekia alikuwa mgonjwa sana, hakujua kama atapona. Alifikiria kwamba atakufa.

Hezekia aliabudu Mungu. Aliamini Mungu. Hezekia alihuzunika sana. Alimgeukia Mungu amsaidie. Nabii Isaya alimwendea Hezekia. Alimletea ujumbe kutoka kwa Mungu. Alimwambia, "Bwana anasema hivi, 'Ambia familia yako na watumishi, wasio yako ya mwisho. Unaenda kufa. Hautapona.'"

Isaya alienda nje ya nyumba. Hezekia aligeuka akaangalia kwa ukuta na kulia. Hezekia aliudhika sana kwa sababu anaenda kufa. Aliomba Mungu, "Kumbuka, Ee Bwana, vile nimekuwa mwaminifu Kwako. Nimekuabudu Wewe na nimefanya mazuri machoni pako."

Hezekia alilala kitandani, akalia na kuomba kwamba Mungu amsaidie awe mzima tena. Mungu alijibu maombi ya Hezekia papo hapo. Isaya alikuwa bado kwa nyumba ya mfalme. Hakukuwa ameenda nyumbani. Mungu alimpa ujumbe wa Hezekia. Isaya alirudi kuambia Hezekia huo ujumbe wa Mungu.



Isaya aliambia Mfalme Hezekia, "Mungu amesikia maombi yako. Mungu ameona machozi yako. Mungu atakuponya. Kwa muda wa siku tatu utakuwa mzima. Utaenda Hekaluni kuabudu Mungu. Mungu ataongeza miaka kumi na tano kwa maisha yako. Mungu atakuokoa wewe na huu mji kutoka kwa Mfalme wa Ashuru."

Hezekia aliuliza Isaya ishara ya kuonyesha kwamba Mungu atamponya. Isaya aliambia Hezekia kwamba Mungu atafanya kivuli cha ubao unao tumika kwa kupima saa kiende mbele au nyuma hatua kumi. Hezekia angeamua kivuli kiende mbele au nyuma. Hezekia aliuliza Mungu afanye kivuli cha ubao kirudi nyuma hatua kumi.

Huo ubao wa kupima saa labda ultengenezwa na babake Hezekia. Jua ikichomoza, nguzo ya huo ubao unatengeneza kivuli kwa mwinuko wa ngazi au daraja. Vile jua inaendelea kwenda juu, kivuli kiliendelea kwa ngazi. Watu walitambua wakati kwa kutumia kivuli cha ngazi. Mungu alifanya kivuli kikarudi nyuma tena hatua kumi. Alibadilisha saa.

Isaya aliambia watumishi wa Hezekia watengeneze bandiko ya tini (tini iliyo sagwa sagwa). Watumishi walitengeneza hiyo bandiko ya tini. Waliweka kwa jipu yenye Hezekia alikuwa nayo ikimuumiza. Hezekia alipona.

Kwa siku tatu, Hezekia alikuwa amepona. Alienda Hekaluni kuabudu na kushukuru Mungu.

Mungu alikuwa amefanya ahadi na Daudi. Mungu aliahidi Daudi kwamba kiti cha enzi cha Yerusalem kitakuwa na mfalme wakati wote. Kila uzao wa Daudi ulikuwa na mwana aliye kuwa mfalme baadaye.

Hezekia hakuwa na mwana. Kama Hezekia angekufa, hakungekuwa na mwanawe wa kukalia kiti kama mfalme baada yake. Mungu alimwongezea miaka mingine kumi na tano kwa maisha yake. Kwa muda huo ndio Hezekia alipata mwana. Huyo mwana ndiye alikuwa mfalme. Mungu alitimiza ahadi yake kwa Daudi.

